

**HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA OFISI YA TAIFA
YA TAKWIMU DKT. ALBINA CHUWA WAKATI WA
UZINDUZI NA USAMBAZAJI WA TAKWIMU ZA PATO
LA TAIFA ZILIZOREKEBISHWA KWA TANZANIA BARA
ULIOFANYIKA TAREHE 19 DESEMBA, 2014 KATIKA
UKUMBI WA KARIMJEE DAR ES SALAAM,**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Waziri wa Fedha; Mhe. Saada
Mkuya (Mb.);

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha; Dkt. Servacius Likwelile,
Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;

Wawakilishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali;

Wawakilishi kutoka Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti;

Wawakilishi kutoka Sekta Binafsi;

Ndugu Wanahabari;

Mabibi na Mabwana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Kwa niaba ya Ofisi ya Taifa ya
Takwimu, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa dhati kwa
kukubali kuja kuzindua na kutangaza rasmi matokeo ya takwimu za
Pato la Taifa zilizorekebisha kwa mwaka wa kizio uliotumia bei za
bidhaa na huduma zilizozalishwa mwaka 2007 kwa Tanzania Bara.
Hii inadhihirisha jinsi unavyoathamini na kujali umuhimu wa takwimu

rasmi hapa Nchini na pia ukiwa ndiye Waziri mwenye dhamana ya kusimamia na kuratibu Takwimu Rasmi hapa Nchini ambazo zinaisadia Serikali katika kupanga mipango ya maendeleo na kufanya maamuzi bora kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kama unavvofahamu, kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu SURA 351, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepewa mamlaka ya kutoa na kusambaza takwimu rasmi ikiwa ni pamoja na kuhakiki ubora wa takwimu rasmi kwa kufuata Miongozo iliyowekwa na Ofisi ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa (UNSD) – Fundamental Principles of Official Statistics. Takwimu za Pato la Taifa ni miongoni mwa takwimu zinazorekebishwa kila baada ya miaka mitano ili kupata hali halisi ya mabadiliko ya Uchumi duniani kwa maana ya shughuli mpya zinazoingia kwenye Uchumi na kutoka kwenye Uchumi kutokana kwa kukua kwa sayansi na Teknojia. (Mfano uzalishaji wa Majembe kiwanda cha Ufi – kutoka katika Uchumi), kuingiza gesi kwenye uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kazi hii ya kurekebisha takwimu za Pato la Taifa kwa Tanzania Bara imetumia Tafiti za Taifa zilizofanyika kwa kipindi cha mwaka 2001 hadi mwaka 2007. Baadhi ya Tafiti hizo ni pamoja na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa Mwaka 2007, Sensa ya Kilimo iliyofanyika mwaka 2008 na Takwimu nyingine za Utawala kutoka katika Wizara na Idara za Serikali. Ukokotoaji wa takwimu hizi umefuata Mifumo ya Umoja wa Mataifa ya kutayarisha takwimu za Pato la Taifa ya Mwaka 1993 na 2008. Na hii ni

kuhahakisha kuwa takwimu hizi zinalinganishwa na takwimu nyingine Duniani (coherence and comparability). Kazi hii ilifanyika kwa kuhusisha Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na ushauri wa Ofisi ya Takwimu ya Denmark, Shirika la Fedha Duniani (IMF), na Benki ya Dunia (WB).

Mhe. Mgeni Rasmi, kazi yangu hapa ni kuihakikishia umma kuwa takwimu hizi ni shirikishi ni bora zaidi katika kufuatilia Sera za Uchumi Jumla na Sera Nyingine kwa kuwa zimeboreshwa zaidi kwa kutumia teknolojia za kisasa katika ukokotoaji, uboreshaji zaidi wa kukusanya takwimu za uchumi katika shughuli za uzalishaji na pia zinatoa hali halisi ya mabadiliko ya kiuchumi hapa Nchini. Nitumie nafasi hii kusema kuwa takwimu hizi zitawekwa katika tovuti ya NBS kwa ajili ya kupanua wigo mpana wa matumizi yake ndani na nje ya Nchi, elimu kwa umma itaendelea kutolewa.

MHESHIMIWA MGENI RASMI, NASHUKURU KWA KUNISIKILIZA.